TMF NI NINI?

Mfuko wa Vyombo vya Habari Tanzania (Tanzania Media Fund-TMF) ni Mfuko unaokusudia kukuza uhuru na ubora wa vyombo vya habari, kwa kujikita zaidi katika habari za maslahi ya umma na uchunguzi. TMF inaamini kuwa vyombo huru vya habari ni roho ya jamii huru na ya kidemokrasia. Ni kwa msingi huu, tunatoa ruzuku kwa waandishi wa habari mmoja mmoja wanaotaka kufuatitilia miradi ya habari za maslahi kwa umma na zile za uchunguzi kote nchini Tanzania bara na Zanzibar.

NANI ANAWEZA KUOMBA RUZUKU?

TMF inawakaribisha waandishi wote walioko Tanzania Bara na/au Zanzibar kuwasilisha mapendekezo ya wazo la kuandika habari zenye maslahi kwa umma au za uchunguzi. Pendekezo la wazo la habari linapaswa kuzingatia misingi ya maadili ya uandishi wa habari, kutoa fursa sawa ya kusikika kwa vyanzo vya habari. Tunakaribisha zaidi wazo la habari linalogusa masuala yaliyoko nje ya Dar es Salaam au nje ya miji, yenye kuakisi upeo wa kina na ubunifu. TMF pia inakaribisha kwa usawa maombi kutoka kwa waandishi wa habari walioko vijijini na waandishi wanawake.

Waombaji wanapaswa angalau kuwa na cheti cha uandishi wa habari au sifa inayofanana na hiyo au angalau uzoefu wa miaka miwili katika kazi ya uandishi wa habari.

VIGEZO VYA KUPATA RUZUKU

TMF itatoa ruzuku kwa michanganuo inayohusu kuandika habari zenye maslahi kwa umma na za uchunguzi.

Vigezo tunavyotumia kutathmini ubora wa mchanganuo wa mwombaji ni:

- Upekee au utofauti wa wazo la habari
- Ubora wa utafiti wa awali kuhusiana na wazo la habari.
- Ubora wa mpango kazi wa kiuandishi wa habari wenye utafiti unaozingatia vyanzo vingi tofauti vya habari vyenye uwiano sawa
- Mbinu za kiuandishi za utafutaji wa habari zitakazowezesha kupata habari iliyokusudiwa
- Uwezekano wa kutumika kwa habari iliyo bora katika chombo cha habari ili kuongeza ubora wa habari

Mchanganuo sharti uzingatie kuchangia kipaumbele kwa moja ya maeneo yafuatayo:

- kuongeza uwazi na uwajibikaji katika jamii na kuchochea mijadala ya hoja.
- kuongeza wigo wa kusikika kwa sauti za wananchi hususani walioko vijijini na wanyonge au waliosahaulika.
- Kuleta ufumbuzi wa kiini cha umaskini Tanzania.

Maelezo kamili kwa ruzuku za aina mbalimbali yapo upande wa pili.

NAMNA YA KUTUMA MAOMBI

Unaweza kupata fomu ya maombi toka ofisini kwetu au ichukue kwenye tovuti yetu: www.tmf.or.tz. Unapaswa kutuma nakala moja ya maombi yaliyokamilika ukiambatanisha a) maelezo yako binafsi (CV), b) picha ya karibuni saizi ya pasipoti, c) sampuli mbili za kazi yako iliyochapishwa, na d) majina ya watu wawili walioko tayari kutoa maelezo yanayokuhusu. Maombi yanaweza kutumwa kwa njia ya barua pepe, kwa njia ya posta au kwa kuletwa moja kwa moja ofisini kwetu.

Tanzania Media Fund (TMF)
Mafinga Street, Plot No. 127, Kinondoni
SLP 38266, Dar es Salaam
Tel: +255 22 2664306/07 Faksi: +255 22 2664308

AINA YA RUZUKU BINAFSI

Kuna aina tatu ya ruzuku kwa mwandishi mmoja mmoja: Ruzuku ya chapchap, Ruzuku ya Mkoa na ya Upeo mpana. Mwombaji anaruhusiwa kuomba ruzuku ya aina moja tu kwa kila wakati.

	Ruzuku ya chapchap	**Ruzuku ya Mkoa**
Ukomo wa ruzuku	**Tshs. 500,000**	**Tshs. 1,000,000**
Ukomo wa muda wa kufanya kazi	Mwezi Mmoja	Miezi Mitatu
Ukomo wa muda wa mchakato wa kushughulikia maombi	Wiki 2	**Wiki 6**
Walengwa	Waandishi wanaotaka kuchapisha habari zinazohitaji muda mfupi kufanyiwa kazi.	Waandishi wanaotaka kuchapisha au kufuatilia habari zinazolenga masuala ya vijijini
Madhumuni	Kusaidia upatikanaji wa habari ambazo vinginevyo zisingeweza kupatikana.	Kuvisaidia vyombo vya habari kupata habari za vijijini Kuhamasisha uandishi na ufuataliaji wa habari zinazohusu Ukimwi na masuala ya jinsia
Kutoa Ripoti	Wiki 2 baada ya kumaliza kazi	Wiki 2 baada ya kumaliza kazi
Muda wa Kutoa Ruzuku	Mara zote katika mwaka	Mara tatu kwa mwaka. Idadi inaweza kuongezeka kulingana na uhitaji.

TMF HAIVUMILII RUSHWA KAMWE .
TUPE TAARIFA KWA SIRI VIASHIRIO VYA RUSHWA KWA RUZUKU ZA TMF KUPITIA concern@tmf.or.tz AU SIMU +255 22 2664306/07.

Tarehe ya Maombi:

SEHEMU YA 1: MAELEZO YA MWOMBAJI NA WADHAMINI

PICHA

A: Maelezo binafsi ya Mwombaji

- Majina kamili…….
- Jinsia……
- Tarehe ya Kuzaliwa…….
- Mahali pa kuzaliwa……...
- Mkoa unaoishi……...
- Wilaya unayoishi……
- Mtaa unaoishi…….
- Namba ya nyumba unayoishi…….

B: Mawasiliano ya Mwombaji

- Namba ya simu ya mezani…….
- Namba ya simu ya kiganjani……..
- Barua pepe…….
- Namba ya faksi……..
- Sanduku la posta……

C: Maelezo binafsi na mawasiliano ya mdhamini mwenye taaluma ya habari

- Jina la mdhamini mwenye taaluma ya habari……..
- Namba ya simu ya mezani ya mdhamini ……
- Namba ya simu ya kiganjani ya mdhamini……...
- Barua pepe ya mdhamini……..
- Namba ya faksi ya mdhamini……
- Sanduku la posta la mdhamini……..
- Kazi anayofanya mdhamini……...
- Uhusiano wako wa kikazi/kitaaluma na mdhamini..…….

D: Maelezo binafsi na mawasiliano ya mdhamini mwenye taaluma ya habari

- Jina la mdhamini ……..……..
- Namba ya simu ya mezani ya mdhamini ……
- Namba ya simu ya kiganjani ya mdhamini……...
- Barua pepe ya mdhamini……..
- Namba ya faksi ya mdhamini……
- Sanduku la posta la mdhamini……..
- Kazi anayofanya mdhamini……...
- Uhusiano wako wa kikazi/kitaaluma na mdhamini..…….

E: Tafadhali ambatanisha maelezo binafsi (CV) na vyeti vyako hususan vya kitaaluma.

SEHEMU YA 2: WAZO LA HABARI, MAKUBALIANO, AINA YA RUZUKU NA KIPAUMBELE

A: Wazo la Habari: Kwa ufupi nini wazo lako moja la habari ambalo ungependa kulifanyia kazi inayohusiana na habari za uchunguzi au matakwa ya jamii……
……
……
……

B: Makubaliano ya msingi kutoa habari

Maombi yako ya ruzuku ni kwa ajili ya kukuwezesha kufanya kazi ya uandishi wa habari ambayo isingewezekana hususan kufika katika maeneo au kuibua masuala yaliyofichika bila ruzuku. Makubaliano ya msingi ni kuthibitisha kuwa una mawasiliano na chombo chako cha habari kuhusiana na wazo la habari unalotaka kufanyia kazi na kwamba hatimaye habari zako zitatumika katika chombo hicho cha habari ili kwa pamoja tuweze kuongeza uwingi na ubora wa habari.

- Jina la chombo unachotoa habari zako kila mara…….
- Sema kama chombo hicho ni gazeti, jarida, luninga au redio……..
- Jina la chombo unachokusudia kutoa habari zako ukipata ruzuku……
- Sema kama chombo hicho ni gazeti, jarida, luninga au redio……
- Ambatanisha habari zako za hivi karibuni (angalau kati ya kipindi cha miezi 3-6) zilizotumika katika chombo cha habari unachokusudia kupeleka habari zako (kama ni redio au televisheni, ambatanisha CD).
- Waweza kuthibitisha kwa kuambatanisha barua iliyosainiwa na mhariri wa chombo husika na kupigwa mhuri ikieleza kufahamu juu ya wazo lako la habari na utayari wa kutumia habari zitakazotokana na wazo hilo.
- Hata hivyo, uhakika mdogo wa kutumika kwa habari katika chombo cha habari hakuzuii kupitisha wazo la habari linalothibitika kuwa la kipekee ambalo lenyewe linajitosheleza kukubalika kutumika na chombo kingine chochote.

C: Uharaka Iwapo unaomba ruzuku ya chapchap, tafadhali eleza kwa ufupi uharaka wa kufanyia kazi wazo lako.	**D: Aina ya Ruzuku** Weka alama kwenye aina ya ruzuku unayoomba (Unaruhusiwa kuchagua aina moja tu kwa wakati mmoja)		
	1. Ruzuku ya chapchap	**1.**	
	2. Ruzuku ya mkoani	**2.**	

E: Kipaumbele

Ni eneo gani kati ya maeneo ya kipaumbele hapa chini habari yako ikikamilika itachangia ? (Weka alama kwenye kisanduku husika)

☐	Kuongeza uwazi na uwajibikaji katika jamii na kuchochea mijadala ya hoja.
☐	kuongeza wigo wa kusikika kwa sauti za wananchi hususani walioko vijijini na/au watu ambao kihistoria wametengwa au kusahaulika na wanyonge.
☐	Kuleta ufumbuzi wa kiini hasa cha umaskini Tanzania.

SEHEMU YA 3: MAELEZO YA KINA YA WAZO LA HABARI

[1] Tafadhali toa maelezo ya kina kuhusiana na wazo lako la habari kwa kufuata mwongozo wa maswali hapa chini. Ambatanisha maelezo yako katika karatasi tofauti:-

A: Nini lengo bayana la kufanyia kazi wazo lako la habari
B: Nini utafiti wa awali kuhusiana na wazo lako la habari?
C: Ni maswali gani ya msingi au ya kiutafiti hayajajibiwa katika utafiti huo wa awali ambayo ungependa kufanyia kazi ili kupata habari mpya/tofauti/kipekee?
D: Vyanzo gani muhimu vitakuwezesha kupata habari inayotokana na wazo lako la habari? (zingatia vyanzo vinavyotokana na nyaraka, watu na tovuti)
E: Kwa nini unadhani kuwa wazo hilo ni muhimu kihabari na namna gani litachangia moja ya maeneo ya kipaumbele katika sehemu ya 2E?

SEHEMU YA 4: MPANGO KAZI

Eleza mpango kazi wako kwa mpangilio utakaokuwezesha kufikia hatua ya mwisho ya kuandika habari na kuitoa katika chombo cha habari. Ambatanisha mpango kazi wako kwa kufuata mfano huu chini:-

A: Nini na Lini utafanya

Nini utafanya?	**Lini utafanya?**

B: Muda na Idadi ya Habari utakazotoa

[1] Wazo lako la habari ni muhimu lihusiane na uandishi wa habari za uchunguzi ambao ni ule **makini** na wa **kina**. **Makini** maana yake ni uandishi usiotoa taarifa ya matukio tu, bali huibua habari ambazo vinginevyo zisingeweza kuwapo bila mwandishi wa habari kuzifanyia kazi. **Za Kina** inamaanisha kuwa kuna kazi ya ziada ya kiuandishi inahitajika, (mathalani kwa urefu wa muda uliotumika kwenye utafiti au, idadi ya watoa habari waliofikiwa) au kwa maana ya ubora (mathalani, ubora wa maswali yaliyoulizwa, mbinu mpya zilizotumika, au yote mawili.

- Tarehe ya kuanza kazi……
- Tarehe ya kumaliza kazi…….
- Tarehe ya kutoa habari kwenye chombo cha habari……..
- Idadi ya siku utakazotumia kufanya kazi……..
- Idadi ya habari utakazotoa katika chombo cha habari……..

SEHEMU YA 5: BAJETI

Kutekeleza mpango kazi wako ni gharama. Kumbuka wewe au chombo unachofanyia kazi mna wajibu pia kuchangia gharama hizo. Hakikisha gharama zinazotokana na mpango kazi hapo juu zinaonekana katika bajeti kama ilivyoainishwa hapa chini. Ni muhimu kuwa na uhakika wa nauli ya usafiri utakaoutumia na siku utakazofanya kazi. Tumia jedwali hapa chini kwa bajeti ya mpango kazi wako.

Kipengele cha bajeti	**Siku ngapi/ Ngapi**	**Gharama kwa kila moja/ siku**	**Jumla ya gharama**
Posho ya kujikimu[2]			
Usafiri			
Mawasiliano ya simu			
Gharama nyingine[3]			
Jumla ya Gharama			

[2] **Posho ya kujikimu kwa siku ni shilingi 65,000/- (hii inajumuisha gharama za usafiri wa ndani ya eneo husika unalofuatilia habari, chakula pamoja na malazi).**

[3] Gharama nyingine ni zile ambazo hazikutajwa hapo juu, iwapo ni muhimu katika kutekeleza kazi yako**.**

SEHEMU YA 6: DOKEZO LA JUMLA:

Maofisa wa TMF mara wapitiapo maombi yako na kubaini mapungufu yanayoweza kukunyima usawa wa ushindani wa kupata ruzuku hulazimika kuwasiliana na mwombaji kumtaka atoe maelezo yaliyopungua. Kufanya hivyo haina maana ya kukusumbua bali kukusaidia ushindane kwa usawa. Pia haina maana ya kukujengea matumaini makubwa ya kupata ruzuku. Unapokosa ruzuku pamoja na kukuomba maelezo yaliyokuwa yamepungua amini ni sehemu ya ushindani. Hata hivyo, kabla ya kutuma maombi yako ni vema ujikague kama kila kitu kipo sawa kwa kuweka alama ya vema mbele ya kila dondoo hapa chini:-

Na.	Dondoo	Alama
1	Umetaja tarehe ya maombi na kubandika picha yako?	
2	Umetoa maelezo binafsi ya mwombaji kikamilifu?	
3	Umetoa mawasiliano ya mwombaji kikamilifu?	
4	Umetoa kikamilifu maelezo binafsi na mawasiliano ya wadhamini wako ni vema wakiwa wenye taaluma ya habari ?	
5	Umetaja wazo lako la habari linaloeleweka?	
6	Umetaja jina la chombo cha habari unachotoa habari zako kila mara?	
7	Umesema kama chombo hicho ni gazeti,jarida,luninga au redio?	
8	Umetaja jina la chombo cha habari unachokusudia kutoa habari zako?	
9	Umesema kama chombo hicho ni gazeti, jarida, luninga au redio?	
10	Umeambatanisha CV yako?	
11	Umeambatanisha vyeti vyako au kama hauna vyeti kazi zako kadhaa zilizotoka mfululizo hivi karibuni katika moja ya chombo cha habari?	
12	Umeambatanisha barua ya mhariri inayothibitisha uwezekano wa kutoa habari yako katika chombo chake?	
13	Umetaja aina ya ruzuku unayoomba na kuhakikisha hujaomba ruzuku zaidi ya aina moja?	
14	Iwapo umeomba ruzuku ya chapchap umeeleza sababu ya uharaka wa kufanyia kazi wazo lako?	
15	Umetaja wazo lako linaangukia kipaumbele gani?	
16	Umetoa maelezo ya kina ya wazo lako kwa kujibu maswali A, B, C, D na E	
17	Katika mpango kazi wako, umeeleza nini utafanya na lini utafanya?	
18	Umejaza kikamilifu muda na idadi ya habari utakazotoa?	
19	Katika bajeti yako, umezingatia posho ya kujikimu kwa siku ni shilingi elfu 65?	
20	Umehakiki nauli halisi kwenda maeneo utakayofanyia kazi?	
21	Umehakiki gharama nyingine ulizotaja zimeainishwa katika mpango kazi?	
22	Umewahi kuomba ruzuku ya TMF kabla? Sema: **Ndiyo** au **Hapana**	
23	Iwapo jibu ni Ndiyo swali namba 22, umekwishalipwa asilimia 20 iliyobaki? Sema: **Ndiyo** au **Hapana**	